

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO

Simu: +255 (028) 2820137  
Fax: +255 (028) 2820137  
Unapojibu tafadhali taja:



S. L. P 03,  
**KAKONKO.**

**Kumb.Na.HW/KNK/S.40/VOL2/15**

9.03. 2020.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko, Mkoani Kigoma, kupitia Kibali cha Ajira Mbadala **Kumb. Na. FA.17/358/01/"B"/49** cha tarehe 23 Januari, 2020 kilichotolewa na Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, anapenda kuwatangazia wananchi wote wa Tanzania wenye sifa za kuajiriwa katika Utumishi wa Umma kuleta maombi ya kazi kwa nafasi ya Mtendaji wa Kijiji III kama ifuatavyo:

### **Mtendaji wa Kijiji III - Nafasi 1**

#### **MAJUKUMU YA KAZI:**

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji wa Shughuli zote za Kijiji.
- ii. Katibu wa Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji, Mtunzaji wa kumbukumbu zote za kijiji za vikao vya Kijiji pamoja na hati ya kuandkishwa Kijiji, mali za kijiji, na rejesta ya kijiji nk.
- iii. Kuratibu na kusimamia na kuhamasisha upangaji na utekelezaji wa shughuli zote na Mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- iv. Kusimamia ulinzi na Utawala Bora wa wananchi (Mlinzi wa amani) katika Kijiji.
- v. Kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo katika Kijiji.
- vi. Kupanga na kuhakikisha kupitishwa kwa ratiba za vikao vya mkutano mkuu na Halmashauri ya Kijiji.
- vii. Kuandaa taarifa mbalimbali za Halmashauri ya kijiji kwa ajili ya mkutano mkuu wa kijiji.
- viii. Msimamizi wa mapato na kodi za kijiji.
- ix. Mfuatiliaji wa miradi ya kijiji na kutoa taarifa kwenye halmashauri ya kijiji.

#### **NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali ngazi ya mshahara TGS B, Tsh 390,000 hadi Tsh 489,000. Atanza na Mshahara wa Tsh 390,000/= kwa mwezi

#### **SIFA ZA MWOMBAJI**

Wahitimu wa kidato cha nne au sita waliohitimu mafunzo ya astashahada / cheti katika (Tech. level 5) au kinachofanana na hicho mojawapo ya fani zifuatazo: Utawala, Maendeleo ya Jamii, Sheria, Uongozi na Fedha kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali.


Maombi yote yatumwe kupitia anwani ifuatayo :

**MKURUGENZI MTENDAJI(W)**  
S.L.P 03,  
Kakonko

**MASHARTI YA JUMLA**

Mwombaji anatakiwa kutimiza masharti yafuatayo kikamilifu:

- i. Awe ni Raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45, bila kujali jinsi, ulemavu, kabila, dini au hali.
- ii. Aambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa na Maelezo Binafsi (CV) yaliyojitosheleza kwa maana ya taarifa na mawasiliano. Pia aambatanishe picha 1 "Passport Size" iliyochukuliwa hivi karibuni na nakala za vyeti vya Taaluma (Academic) na Weledi (Professional). Transcript "Testimonials" na "Provisional Results" au Statement of Results havipokelewi.
- iii. Maombi yawasilishwe kabla au mnamo tarehe 24/03/2020 saa 9:30 Alasiri. Maombi yatakayowasilishwa baada ya tarehe na muda uliopangwa hayatafanyiwa kazi.

  
Masumbuko S. Magang`hila,  
Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko

**MKURUGENZI MTENDAJI(W)**  
**HALMASHAURI YA WILAYA**  
**KAKONKO**

**NB: Tangazo hili linapatikana pia kupitia tovuti ya Halmashauri: [www.kakonkodc.go.tz](http://www.kakonkodc.go.tz)**